ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***Supplement No. 20*** ***17st May, 2019***

## *SUBSIDIARY LEGISLATION*

*to the Gazette of the United Republic of Tanzania No.20. Vol.100 dated 17st May, 2019*
Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 394 la tarehe 17/5/2019

SHERIA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA
(SURA 191)

KANUNI

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 230(2)(f))*

# KANUNI ZA USIMAMIZI WA MAZINGIRA ZA KUPIGA MARUFUKU MIFUKO YA PLASTIKI ZA MWAKA 2019

## MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Matumizi.
3 TANGAZO LA SERIKALI NA. 394 la tarehe 17/5/2019

SEHEMU YA PILI
MADHUMUNI

4. Madhumuni ya Kanuni.

SEHEMU YA TATU
ZUIO LA MIFUKO YA PLASTIKI

5. Zuio la mifuko ya plastiki.
6. Zuio la vifungashio vya plastiki.
7. Zuio la leseni mpya.
8. Makosa na adhabu.

SEHEMU YA NNE
MATUMIZI YANAYORUHUSIWA

9. Vifungashio vya plastiki vinavyoruhusiwa.
10. Usimamizi wa taka za vifungashio vya plastiki vinavyoruhusiwa.
11. Viwango vya ubora wa vifungashio vya plastiki vinavyoruhusiwa.
12. Wajibu wa kusimamia vifungashio vya plastiki.

SEHEMU YA TANO
UTEKELEZAJI NA USIMAMIZI WA KANUNI

13. Mamlaka ya Waziri.
14. Utekelezaji na usimamizi shirikishi.
15. Wajibu na majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.
16. Mamlaka ya Wakaguzi wa Mazingira.

SEHEMU YA SITA
MASHARTI YA JUMLA

17. Kurejesha mifuko ya plastiki kwenye nchi ilikotoka.
18. Utaifishaji na uteketezaji wa mifuko ya plastiki.
19. Wajibu wa ukusanyaji taka za chupa za plastiki.
20. Kufifilisha kosa.
21. Amri zinazoweza kutolewa na mahakama.
22. Rufaa kwa Waziri.
23. Rufaa kwa Baraza la Rufaa la Mazingira.
24. Kufutwa kwa Kanuni .

SHERIA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA
(SURA 191)

# KANUNI

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 230(2)(f))*

KANUNI ZA USIMAMIZI WA MAZINGIRA ZA KUPIGA MARUFUKU MIFUKO YA PLASTIKI ZA MWAKA 2019

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zitaitwa Kanuni za Usimamizi wa Mazingira za Kupiga Marufuku Mifuko ya Plastiki za mwaka 2019 na zitaanza kutumika tarehe 01 Juni, 2019.

Matumizi

2. Kanuni hizi zitatumika kwa ajili ya kuzuia uingizaji nchini, usafirishaji nje ya nchi, uzalishaji, uuzaji, usambazaji, uhifadhi na matumizi ya mifuko ya plastiki ndani ya Tanzania Bara.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa pale muktadha utaeleza vinginevyo-

Sura 191

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"mfuko mbadala" maana yake ni mfuko uliotengezwa kutokana na malighafi inayooza au inayoweza kurejelezwa na isiyokuwa na kiwango chochote cha plastiki au malighafi nyingine kama ambavyo Waziri atakavyobainisha;

"Baraza" maana yake ni Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira kama lilivyoanzishwa na Sheria;

"Mkurugenzi Mkuu" maana yake ni Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana na masuala yanayohusiana na Mazingira;

"mfuko wa plastiki" maana yake ni mfuko uliotengenezwa kwa malighafi ya plastiki wenye vishikio au bila vishikio ambao una unene wa aina yo yote kwa ajili ya kubebea bidhaa mbalimbali;

"vifungashio vya plastiki" maana yake ni vifungashio vilivyotengenezwa kwa malighafi ya plastiki kwa ajili

ya kuhifadhi ubora au kuzuia uharibifu wa bidhaa ambavyo vitakuwa na lakiri au alama inayotambulisha bidhaa iliyofungashwa kabla ya kuuzwa, kusambazwa au kuingizwa sokoni;

"vifungashio kwa ajili ya sekta ya kilimo" maana yake ni vifungashio vilivyotengenezwa kwa malighafi ya plastiki mahsusi kwa ajili ya kuhifadhi unyevu shambani au kufungashia miche ya mazao mbalimbali kwenye vitalu au kufunika vijumba kwa ajili ya kukuzia mazao au kilimo cha umwagiliaji au kukusanya, kuhifadhi na kusafirishia mazao;

"vifungashio kwa ajili ya sekta ya ujenzi" maana yake ni vifungashio vilivyotengenezwa kwa malighafi ya plastiki mahsusi kwa ajili ya kubebea bidhaa na vifaa vya ujenzi au kuzuia unyevu kupenya kwenye majengo au mabomba au nyaya au vigae au matanki au majengo ya muda au shughuli nyingine zinazohusiana na sekta ya ujenzi;

"vifungashio kwa ajili ya vyakula" maana yake ni vifungashio vilivyotengenezwa kwa malighafi ya plastiki mahsusi kwa ajili ya kuhifadhi ubora wa chakula ambavyo vitakuwa na lakiri au alama inayotambulisha aina ya bidhaa ya chakula iliyofungashwa kabla ya kuuzwa, kusambazwa au kuingizwa sokoni;

"vifungashio kwa ajili ya bidhaa za viwandani" maana yake ni vifungashio vilivyotengenezwa kwa malighafi ya plastiki mahsusi kwa ajili ya kuhifadhi ubora wa bidhaa za viwandani. Vifungashio hivyo vitakuwa na lakiri au alama inayotambulisha bidhaa iliyofungashwa kabla ya kuuzwa au kusambazwa;

"vifungashio kwa ajili ya huduma za afya" maana yake ni vifungashio vilivyotengenezwa kwa malighafi ya plastiki mahsusi kwa ajili ya kufungasha madawa au vifaa vya upasuaji au matibabu au vifaa vya huduma ya meno au huduma macho au huduma yoyote ya afya;

"vifungashio kwa ajili ya usafi na usimamizi wa taka" maana yake ni mifuko ya plastiki iliyotengenezwa kwa ajili ya kukusanya au kubebea taka ngumu ambapo ukubwa na unene wake utaainishwa kwa amri ya Waziri;

## SEHEMU YA PILI
## MADHUMUNI

Madhumuni ya Kanuni

4. Madhumuni ya Kanuni hizi ni-

(a) kupiga marufuku uingizaji nchini, usafirishaji nje

ya nchi, uzalishaji, uuzaji na matumizi ya mifuko ya plastiki bila kujali unene wake;

(b) kulinda afya ya binadamu na wanyama pamoja na mazingira dhidi ya athari zinazoweza kujitokeza kutokana na matumizi ya mifuko ya plastiki; na

(c) kutoa motisha kwa ajili ya kuhamasisha uzalishaji na uingizaji nchini wa mifuko mbadala.

## SEHEMU YA TATU
## ZUIO LA MIFUKO YA PLASTIKI

Zuio la mifuko ya plastiki

5. Mifuko yote ya plastiki kwa ajili ya kubebea bidhaa mbalimbali, bila kujali unene wake, imepigwa marufuku kuingizwa nchini, kusafirishwa nje ya nchi, kuzalishwa, kuuzwa, kuhifadhiwa, kusambazwa na kutumika ndani ya Tanzania Bara.

Zuio la vifungashio vya plastiki

6. Bila kuathiri masharti ya kanuni ya 5, ni marufuku kwa mtu yeyote kuuza vinywaji au bidhaa nyingine zikiwa zimefungashwa kwenye vifungashio vya plastiki isipokuwa tu kama aina ya bidhaa hizo inalazimu kutumia vifungashio vya plastiki.

Zuio la leseni mpya

7. Ni marufuku wa Mamlaka yoyote kusajili au kutoa leseni au kibali kwa mtu yeyote kwa ajili ya kuingiza nchini, kusafirisha nje ya nchi, kuzalisha au kuuza mifuko ya plastiki ambayo imepigwa marufuku kwa mujibu wa Kanuni hizi.

Makosa na adhabu

8. Mtu yeyote atakayeingiza nchini au kusafirisha nje ya nchi au kuzalisha au kuuza au kuhifadhi au kusambaza au kumiliki au kutumia mifuko ya plastiki na vifungashio vya plastiki kinyume na Sehemu hii,atakuwa ametenda kosa, na endapo akitiwa hatiani atahukumiwa kama ifuatavyo-

(a) kitendo cha kuzalishaji au kuingizaji nchini wa mifuko ya plastiki, adhabu yake ni faini isiyopungua shilingi milioni ishirini lakini isiyozidi shilingi bilioni moja au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja;

(b) kitendo cha kusafirisha nje ya nchi mifuko ya plastiki, adhabu yake ni faini isiyopungua shilingi milioni tano lakini isiyozidi shilingi milioni ishirini au kifungo kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja;

(c) kitendo cha kuhifadhi au kusambaza mifuko ya plastiki, adhabu yake ni faini kisichopungua shilingi milioni tano lakini isiyozidi shilingi milioni hamsini au kifungo kisichozidi miaka

miwili au vyote kwa pamoja;

(d) kitendo cha kuuza mifuko ya plastiki, adhabu yake ni faini isiyopungua shilingi laki moja na lakini isiyozidi shilingi laki tano au kifungo kisichozidi miezi mitatu au vyote kwa pamoja;

(e) kitendo cha kumiliki au kutumia mifuko ya plastiki, adhabu yake ni faini isiyopungua shilingi elfu thelathini lakini isiyozidi shilingi laki mbili au kifungo kisichozidi siku saba au vyote kwa pamoja.

SEHEMU YA NNE
MATUMIZI YANAYORUHUSIWA

Vifungashio vya plastiki vinavyoruhusiwa

9. Bila kuathiri masharti ya kanuni ya 5, vifungashio vya plastiki kwa ajili ya huduma za afya au bidhaa za viwandani au sekta ya ujenzi au sekta ya kilimo au vyakula au usafi na udhibiti wa taka havitahusika na zuio la Kanuni hizi.

Usimamizi wa taka za vifungashio vya plastiki

TS Na. 263 la mwaka 2009 na 264 la mwaka 2009

10. Mtu yeyote anayeingiza nchini, kusafirisha nje ya nchi, kuzalisha, kuuza, kuhifadhi, kusambaza, kumiliki au kutumia vifungashio vya plastiki ambavyo havijazuiwa na Kanuni hizi ana wajibu wa kuhakikisha kwamba taka zitokanazo na vifungashio hivyo zinasimamiwa kwa mujibu wa Kanuni za Usimamizi wa Taka Ngumu za mwaka 2009 na Kanuni za Usimamizi wa Taka Hatarishi za mwaka 2009.

Viwango vya ubora wa vifungashio vya plastiki vinavyoruhusiwa

11.-(1) Mtu ye yote anayeingiza nchini, anayesafirisha nje ya nchi au anayezalisha vifungashio vya plastiki ambavyo havijazuiwa na Kanuni hizi atahakikisha kwamba vifungashio hivyo vinakidhi viwango vya ubora vilivyowekwa na Shirika la Viwango Tanzania.

(2) Waziri atahamasisha uzalishaji na matumizi ya mifuko na vifungashio mbadala.

Wajibu wa kusimamia vifungashio vya plastiki kwenye vinywaji

TS Na 263 la mwaka 2009

12. Kwa mujibu wa kanuni ya 6, mtu yeyote atakayeingiza nchini, atakayezalisha, atakayesambaza au atakayeuza bidhaa zilizofungashwa kwenye vifungashio vya plastiki atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba taka za vifungashio hivyo zinasimamiwa au kutupwa kwa mujibu wa Kanuni za Usimamizi wa Taka Ngumu za mwaka 2009.

SEHEMU YA TANO
UTEKELEZAJI NA USIMAMIZI WA KANUNI

Mamlaka ya Waziri

13.-(1) Waziri anaweza kwa nyakati tofauti kutoa miongozo, amri au maagizo mbalimbali kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa Kanuni hizi.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Waziri-

(a) kwa kushauriana na Waziri wa Fedha, anaweza kutoa motisha kwa ajili ya kuhamasisha uzalishaji na uingizaji nchini wa mifuko mbadala au uanzishaji wa viwanda vya kurejeleza mifuko inayoruhusiwa na vifungashio vya plastiki ambavyo havijazuiwa na Kanuni hizi;

(b) anaweza kuteua Wakaguzi wa Mazingira katika vituo vya forodha vya mipakani kwa ajili ya kuhakikisha utekelezaji na usimamizi wa Kanuni hizi.

Utekelezaji na usimamizi shirikishi

14. Baraza kwa kushirikiana na Wizara yenye dhamana ya Viwanda na Biashara, Mamlaka ya Mapato (TRA), Mamlaka ya Bandari, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, Jeshi la Polisi, Mamlaka ya Chakula na Dawa, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Shirika la Viwango (TBS), Idara ya Uhamiaji na taasisi nyingine za Serikali, katika kutekeleza majukumu yake ya kisheria, litahakikisha linatekeleza na kusimamia Kanuni hizi.

Wajibu na majukumu ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

15. Mamlaka za Serikali za Mitaa, pamoja na majukumu waliyonayo kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Usimamizi wa Taka Ngumu za mwaka 2009 katika usimamizi wa taka, zitatakiwa-

(a) kuhakikisha utekelezaji na usimamizi wa Kanuni hizi; na

(b) kuendesha programu za elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa zuio la matumizi ya mifuko ya plastiki pamoja na athari zake kwa afya ya binadamu na mazingira.

Mamlaka ya Wakaguzi wa Mazingira

16. Wakaguzi wa Mazingira watatumia mamlaka na wajibu wao waliyopewa kisheria kuhakikisha uzingatiwaji na utekelezaji na usimamiziwa Kanuni hizi.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI YA JUMLA

Kurejesha mifuko ya plastiki kwenye nchi ilikotoka

17. Shehena ya mifuko ya plastiki iliyozuiliwa au vifungashio vya plastiki vinavyoruhusiwa na Kanuni hizi ikipatikana katika kituo chochote cha mpakani kinyume na masharti ya Kanuni hizi, itarejeshwa katika nchi ilikotoka kwa gharama za mwagizaji wa shehena hiyo.

Utaifishaji na utupaji wa mifuko ya plastiki

18.-(1) Bila kuathiri masharti ya kanuni ya 17, mifuko ya plastiki itakayobainika kuwepo kinyume cha masharti ya Kanuni hizi itataifishwa na kuteketezwa au kurejelezwa kwa njia zilizo rafiki kwa mazingira chini ya usimamizi wa Baraza au Wakaguzi wa Mazingira kwa gharama za mtenda kosa.

(2) Mamlaka husika zitahakikisha kuwa mifuko ya plastiki itakayoingizwa nchini kinyume na masharti ya Kanuni hizi itataifishwa na kuteketezwa au kurejelezwa kwa njia zilizo rafiki kwa mazingira chini ya usimamizi wa Baraza au Wakaguzi wa Mazingira.

Wajibu wa ukusanyaji taka za chupa za plastiki

19. Bila kuathiri masharti ya kanuni ya 5, mzalishaji yeyote au msambazaji wa bidhaa zilizofungashwa katika chupa za plastiki ataweka utaratibu wa kuendesha au kushiriki katika mfumo wa kukusanya taka za chupa za plastiki zinazotokana na bidhaa zake kwa ajili ya kurejeleza na haruhusiwi kuongeza bei kwa mlaji ili kufidia gharama ya huduma hiyo.

Kufifilisha kosa

20.- (1) Mkurugenzi Mkuu wa Baraza au Mkaguzi wa Mazingira kwa madhumuni ya kutekeleza Kanuni hizi, anaweza kufifilisha kosa chini ya Kanuni hizi kwa mtu yeyote atakayeonesha nia ya kulipa kiasi chochote cha pesa kama faini kutokana na kukiuka masharti ya Kanuni hizi.

(2) Bila kuathiri mashati ya kanuni ndogo ya (1), mtu yeyote aliyeteuliwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Kanuni hizi, anaweza kufifilisha kosa lililotendwa chini ya kanuni ya 8(e) kwa mtu yeyote anayeonesha nia ya kulipa kiasi cha fedha atakachotozwa kama adhabu.

(3) Kwa kuzingatia kanuni ya 8, hakutakuwa na adhabu nyingine zitakazotolewa dhidi ya mtu ambaye mamlaka ya kufifilisha kosa yameshatekelezwa dhidi ya mtu huyo.

Amri zinazoweza kutolewa na mahakama

21. Pamoja na adhabu nyingine zitakazotolewa chini ya Kanuni hizi, Mahakama inaweza kutoa amri zifuatazo:

(a) kutaifisha mifuko ya plastiki;
(b) kufunga kiwanda kinachozalisha mifuko ya plastiki;
(c) kufuta leseni; au
(d) kuamrisha kushiriki katika kutoa huduma za kijamii.

Rufaa kwa Waziri

22. Mtu yeyote ambaye hakuridhika na uamuzi uliotolewa kwa mujibu wa Kanuni hizi, isipokuwa uamuzi wa mahakama, anaweza kukata rufaa kwa Waziri ndani ya siku thelathini kutoka siku ya maamuzi.

Rufaa kwa Baraza la Rufaa la Mazingira

23. Mtu yeyote ambaye hakuridhika na uamuzi utakaotolewa na Waziri, anaweza kukata rufaa kwenye Baraza la Rufaa la Mazingira ndani ya siku thelathini kwa namna ambavyo itawekwa na Baraza.

Kufutwa kwa Kanuni za mwaka 2015

24. Kanuni za Kudhibiti Mifuko ya Plastiki za mwaka 2015 zinafutwa.

Dodoma,
23rd May, 2019

JANUARY Y. MAKAMBA
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira)*